HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA

Simu Namba: 023 2410210
: 023 2410251
Faksi Namba: 023 2410211
Barua Pepe:ded@newaladc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Wilaya ya Newala,
Sanduku La Posta 16,
NEWALA – MTWARA.

08/05/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala amepokea Kibali cha Ajira Mbadala toka kwa Katibu Mkuu OR – Utumishi chenye Kumb. Na. FA.170/372/01/77 cha tarehe 9/4/2020, hivyo anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kazi zifuatazo:-

1. Katibu Mahsusi III (Nafasi 1).
2. Mtendaji wa Kijiji III (Nafasi 1).

1. KATIBU MAHSUSI III – NAFASI 1

SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe raia wa Tanzania.
- Mwombaji awe na akili timamu.
- Awe amehitimu kidato cha nne (IV).
- Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa hatua ya tatu.
- Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja.
- Awe amepata mafunzo kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

KAZI ZA KUFANYA

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
2. Kusaidia kupokea wageni, kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.

3. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
4. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
5. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote zinazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
6. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
7. Kutekeleza kazi nyingine atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

NGAZI YA MSHAHARA

Atakayefaulu usajili na kuajiriwa atalipwa mshahara ngazi ya TGS B_1 kwa mwezi.

2. MTENDAJI WA KIJIJI III – NAFASI 1

SIFA ZA MWOMBAJI

- Mwombaji awe raia wa Tanzania.
- Mwombaji awe na akili timamu.
- Awe amehitimu elimu ya kidato cha Nne au Sita.
- Awe amehitimu Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo – Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI ZA KUFANYA

1. Katibu wa Kamati ya Kijiji.
2. Mtendaji Mkuu wa Kijiji.
3. Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Kijiji.
4. Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu mipango ya maendeleo katika Kijiji,
5. Msimamizi wa Sheria Ndogo pamoja Sheria nyingine zinazotumika katika Kijiji.
6. Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.

7. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uongozi wa njaa na umaskini katika Kijiji.
8. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wakati wote. Kuandaa na kutunza rejesta za wakazi wote wa Kijiji.

NGAZI YA MSHAHARA

Atakayefaulu usajili na kuajiriwa atalipwa mshahara ngazi ya TGS B_1 kwa mwezi.

TARATIBU ZA KUTUMA MAOMBI

1. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na iambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, taaluma na CV (Curriculum Vitae), cheti cha kuzaliwa na picha moja ya passport size ya hivi karibuni.
2. Barua iandikwe namba za simu za mwombaji za kiganjani.
3. **Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45**
4. Kwa walioajiriwa maombi yapitishwe na Waajiri wao wa sasa.
5. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/5/2020 saa 9: 30 Alasiri siku ya Alhamisi saa 9:30 alasiri.
6. Waombaji waandike majina yao yote matatu kwa kirefu.

Barua za maombi ya kazi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Newala,
Sanduku la Posta 16,
NEWALA.

Tangazo limetolewa na

Mussa M. Chimae
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA YA NEWALA

Nakala: Katibu Tawala Mkoa,
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
Sanduku la Posta 544,
MTWARA.

" Mkurugenzi wa Manispaa,
MTWARA – MIKINDANI.

" Mkurugenzi wa Mji,
NEWALA, NANYAMBA NA MASASI.

" Mkurugenzi Mtendaji (W),
TANDAHIMBA, MASASI, MTWARA NA NANYUMBU.

" Mbao za matangazo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA

Simu Namba: 023 2410210
: 023 2410251
Faksi Namba: 023 2410211
Barua Pepe:ded@newaladc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Wilaya ya Newala,
Sanduku La Posta 16,
NEWALA – MTWARA.

08/05/2020

TANGAZO LA NAFASI YA AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala anatarajia kuajiri Msaidizi wa Hesabu II katika ngazi ya Kituo cha Afya ili kuboresha utoaji wa huduma za Afya na usimamizi wa fedha katika Vituo vya Afya hivyo anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kazi ifuatayo:-

1. MSAIDIZI WA HESABU II – NAFASI MOJA (1)

Ngazi ya mshahara ni TGS. B_1 kwa mwezi.

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na akili timamu.
- Awe amehitimu kidato cha nne (IV).
- Awe na cheti cha kuzaliwa.
- Mwombaji awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Awe na cheti cha Astashahada ya Uhasibu kutoka chuo kinachotambulika na Serikali au cheti cha ATEC I kinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA.

KAZI ZA MAJUKUMU

1. Kuandika na kutunza rejesta zinazohusu shughuli za uhasibu.
2. Kuandaa hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha.
3. Kupeleka barua/ nyaraka za uhasibu benki.
4. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

Maombi yaambatanishwe na maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti, picha za ''passport size'' mbili za hivi karibuni, wadhamini watatu, anwani za wadhamini na namba zao za simu.

Barua zote ziandikwe namba za simu za kiganjani za muombaji, kwa wale walioajiriwa maombi yao yapitishwe na mwajiri wake wa sasa na Waombaji waandike majina yao yote matatu kwa kirefu.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/5/2020 saa 9: 30 Alasiri.

Barua za maombi ya kazi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Newala,
Sanduku la Posta 16,
NEWALA.

Tangazo hili limetolewa na:

Mussa M. Chimae
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA YA NEWALA